**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA MALIASILI NA UTALII**

## CHUO CHA VIWANDA VYA MISITU

# TANGAZO LA KUJIUNGA NA CHUO KWA MWAKA WA MASOMO 2025/2026

Mkuu wa Chuo cha Viwanda vya Misitu (FITI)-Moshi anautangazia umma kuwa dirisha la pili la kupokea maombi ya kujiunga na chuo kwa mwaka wa masomo 2025/2026 limefunguliwa. Muda wa kutuma maombi kwa awamu ya pili ni kuanzia tarehe **19 Julai, 2025** hadi tarehe **30 Septemba, 2025**.

## 1. KOZI ZITOLEWAZO

(a) Astashahada ya awali ya Teknolojia ya Viwanda vya Misitu (NTA 4) mwaka mmoja
(b) Astashahada ya Teknolojia ya Viwanda vya Misitu (NTA 5) mwaka mmoja
(c) Stashahada ya Teknolojia ya Viwanda vya Misitu (NTA 6) mwaka mmoja

## 2. SIFA ZA MWOMBAJI

(a) **Astashahada ya awali ya Teknolojia ya Viwanda vya Misitu (NTA Level 4):** Mwombaji awe amehitimu kidato cha nne (O-Level) na ufaulu wa alama D katika masomo manne. Mawili kati ya masomo aliyofaulu yawe ni Bailojia au Kemia au Fizikia au Hesabu au Jiografia. Masomo mengine mawili kati ya hayo aliiyofaulu yasiwe dini, ufaulu wa somo la kiingereza utakuwa kipaumbele katika uchaguzi;

(b) **Astashahada ya Teknolojia ya Viwanda vya Misitu (NTA Level 5):** Mwombaji awe na cheti cha kuhitimu astashahada ya awali ya Teknolojia ya Viwanda vya Misitu au astashahada ya awali ya ufugaji nyuki au astashada ya awali ya misitu au fani nyingine inayolandana na hizo kutoka chuo chochote kinacho tambulika na NACTVET au awe amehitimu kidato cha sita na awe amesoma michepuo ya sayansi na kufaulu katika masomo mawili kwa alama ya E na S;

(c) **Stashahada ya Teknolojia ya Viwanda vya Misitu (NTA Level 6):** Mwombaji awe amehitimu astashahada ya Teknolojia ya Viwanda vya misitu au awe amehitimu na kufaulu fani nyingine yoyote ya sayansi inayolandana na hizo kutoka chuo kinacho tambulika na NACTVET;

## 3. JINSI YA KUTUMA MAOMBI

(a) Maombi yatumwe kupitia barua pepe: admision@fiti.ac.tz, au kwa njia ya mtandao kupitia kiunganishi; https://saris.maliasili.go.tz/Registration/23 au kwa kujaza fomu za maombi ya kujiunga na Chuo. Fomu zinapatikana kwenye tovuti ya Chuo http//www.fiti.ac.tz
(b) Gharama ya maombi ya kujiunga na chuo ni Tsh. 20,000.00. Malipo yote yanafanyika kwa kutumia *Control number*. Kupata *control number* au ufafanuzi wasiliana na Afisa udahili wa chuo kwa namba za simu **0768 890 896**

**KUMBUKA:** (i) Mwombaji baada ya kudahiliwa atakuwa na sifa ya kupata mkopo kutoka Bodi ya Mikopo (HESLB)
(ii) Mafunzo ni kwa vitendo zaidi KARIBU UPATE UJUZI WA MISITU

**“FITI TUNASEMA MISITU NI PESA NA AJIRA”**

Imetolewa na:
**Mkuu wa Chuo, Chuo cha Viwanda vya Misitu, S. L. P 1925, Moshi. Tovuti: www.fiti.ac.tz**